JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

MAPITIO YA MFUMO WA HAKI ZA MADAI

YALIYOMO

- Mapitio ya Mfumo wa Haki ya Madai
- Jukumu la Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania katika Utatuzi wa Migogoro ya Kibiashara
- Maeneo ya Mkazo Wakati wa Kutafuta Maoni
- Mafanikio ya Mapitio ya Mfumo wa Haki za Madai

HISTORIA FUPI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa msaada wa wafadhili, inatekeleza Programu ya Maboresho ya Mazingira ya Biashara Tanzania. Lengo kuu la programu hii ni kuboresha shughuli na ushindani wa biashara, kwa kuanzisha njia rahisi na sahihi za kudhibiti mazingira ya kibiashara nchini Tanzania. Baraza la Mawaziri liliidhinisha kuanzishwa kwa programu hii Julai mwaka 2002 na ilianza kutekelezwa rasmi February mwaka 2004. Mwanzoni, programu hii ilifadhililiwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Denmark, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza, Shirika la Ushirikiano la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden na Ubalozi wa Uholanzi. Baada ya mwezi Januari ya Mwaka 2006, Benki ya Dunia nayo ilijiunga kufadhili programu hii na kuwezeshwa kuanzishwa kwa Mradi wa Ushindani wa Sekta Binafsi ambao inahusisha sehemu tatu zifuatazo:-

1. Maboresho ya Mazingira ya Biashara Tanzania, Programu ya Kujenga Mazingira Bora ya Biashara.
2. Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania kwa ajili ya maendeleo ya sekta binafsi.
3. Mfuko wa Sekta ya Fedha wa Kusaidia Upatikanaji wa Fedha.

Programu ya Maboresho ya Mazingira ya Biashara Tanzania inaratibiwa na Kitengo cha Kanuni Bora ambacho kipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Watekelezaji wakuu wa programu hii ni taasisi za serikali ikiwemo pia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania.

Sehemu Kuu za Programu

Progamu ya Maboresho ya Mazingira ya Biashara Tanzania imegawanyika katika sehemu kuu saba (7) ambazo ni:

1. **Kujiunga, Kuendesha na Kujitoa katika Biashara**
   Sehemu hii inasimamia taratibu za kujiunga, kufanya biashara na kujiondoa kwenye biashara nchini kwa gharama nafuu, kwa haraka na kwa ufanisi. Sehemu hii inasimamiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni.

2. **Maboresho ya Usimamizi wa Ardhi**
   Sehemu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa mfumo bora, fanisi na wa usawa katika usimamizi wa ardhi ili kuhakikisha haki ya kumiliki ardhi inazingatiwa. Sehemu hii ipo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

3. **Utatuzi wa Migogoro ya Kibiashara**
   Sehemu hii inalenga kuhakikisha migogoro ya biashara inatatuliwa kwa wakati, kwa ufanisi, kwa gharama nafuu na kwa urahisi. Sehemu hii ipo chini ya Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria. Watekelezaji wa sehemu hii ni Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria, Idara ya Mahakama, Tume ya Kurekebisha Sheria na Chama cha Mawakili wa Kujitegemea Tanzania Bara.

4. **Maboresho ya Sheria za Kazi**
   Dhumuni la sehemu hii ni kuanzisha utaratibu ambao ni fanisi, wenye kuweza kubadilika kutokana na mazingira na ambao utakubalika katika jamii kiurahisi kwenye masuala ya ajira. Sehemu hii ipo chini ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

5. **Kuimarisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania**
   Dhumuni la sehemu hii ni kusaidia Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania kwa lengo la kuweza kuvutia uwekezaji na kusaidia kujenga mazingira mazuri ya kukuza uchumi nchini.

6. **Uratibu wa Programu ya Maboresho ya Mazingira ya Biashara Tanzania.**
   Sehemu hii inasaidia kitengo kinachohusika na utaratibu wa programu hii kuweza kuratibu programu ili kufanikisha utekelezaji wake kwa ufanisi ili kufikia lengo lililokusudiwa.

7. **Program ya Maboresho ya Mazingira ya Kibiashara Tanzania Zanzibar**
   Sehemu hii ya programu inasimamiwa huko Zanzibar chini ya Wizara ya Fedha na inalenga kuimarisha mazingira ya biashara Tanzania Zanzibar.

MAPITIO YA MFUMO WA HAKI YA MADAI

Mfumo wa haki ya madai ni mfumo ambao unahusika na usimamizi wa haki katika masuala ya madai. Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania inasimamia Mradi huu ambao unalenga katika kufanya mapitio ya mfumo huo kwa kuzingatia miongozo inayohusika, yaani "Miongozo ya msingi ya mapitio ya mfumo wa haki za madai" ambayo ni:

- Kuhakikisha kwamba, wahusika wakuu wa sekta ya sheria wanajihusisha na mapitio ya mfumo wa haki ya madai;
- Kuhakikisha matokeo mazuri ya mapitio na si mapitio yanafanywa ili mradi yafanyike au kuondolewa kabisa kwa sheria husika na kuiga kiujumla maboresho/ marekebisho kutoka sehemu au nchi nyingine;
- Kulenga kwenye mahitaji ya watumiaji wa Mahakama na hasa katika sekta binafsi kwenye masuala ya muda, gharama na mlolongo wa taratibu za madai mahakamani;
- Kuhakikisha kwamba, kuna mahojiano ya kutosha katika kila hatua ya mapitio;
- Kuhakikisha kwamba, utangazaji upo wa kutosha kuhusiana na mapitio hayo ili kuweza kupata ushirikisho na taarifa za kutosha kuboresha mapitio hayo;
- Kuhakikisha kwamba, kuna maafikiano baina ya Majaji, Wasajili, Mahakimu, Mawakili, Madalali na Wahudumu wa Mahakama kuhusiana na lengo la maboresho hayo na;
- Kuhakikisha kwamba, utendaji bora wa kimatifa unazingatiwa ili kuweza kulinganisha uzoefu kutoka nchi nyingine.

Mapitio ya mfumo wa haki ya madai unaangalia ni namna gani miongozo ya misingi ya mapitio katika mfumo wa haki ya madai inavyoweza kufikiwa kama ilivyokusudiwa. Katika kuifanyia kazi miongozo hiyo, maswali yafuatayo yanahitaji kujibiwa;

1. Ni namna gani kanuni za mwenendo wa madai na taratibu zinazohusu mawakili na maafisa wengine wa Mahakama zinavyoweza kuboreshwa ili kuhakikisha kuwa miongozo ya mapitio ya mfumo wa haki za madai zinafanikiwa kama ilivyokusudiwa.
2. Ni kwa namna gani utawala na muundo wa mfumo wa Mahakama unaweza kuboreshwa ili kuhakikisha kwamba miongozo ya mapitio ya mwenendo wa madai inatumika ipasavyo.
3. Ni kwa namna gani, teknolojia ya habari na mawasiliano inavyoweza kutumika ili kuhakikisha kuwa miongozo ya mapitio ya haki ya madai inazingatiwa kama ilivyokusudiwa.

Wadau mbalimbali wa sekta ya Sheria wakimsikiliza Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Mhe. Jaji Prof. Ibrahim Juma wakati wa mkutano wa wadau wa kujadili mfumo wa madai Tanzania chini ya mradi wa BEST.

JUKUMU LA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO YA KIBIASHARA

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ina jukumu la kupitia mfumo wa haki za madai katika sehemu zifuatazo:-

- Kufanya mapitio ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai Tanzania na sheria nyinginezo zinazohusiana na taratibu za madai.
- Kufanya mapitio ya muundo ulipo sasa wa usimamizi wa mashauri wa madai, kuchunguza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwenye Mahakama; na
- Kutoa mapendekezo juu ya marekebisho ya mfumo wa haki za madai ili kuweza kuboresha uharaka na ufanisi wa kutatua migogoro ya madai kwenye Mahakama za Tanzania.

Maboresho katika eneo hili yanalenga kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa ili kuweza kuboresha kasi na huduma zitolewazo na mfumo wa Mahakama kwa wafanyabiashara hao na hasa katika utatuzi wa migogoro ya kibiashara.

Sababu za Mapitio ya Mfumo wa Haki ya Madai

Serikali ya Jumhuri ya Muungano wa Tanzania inalenga kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu wote na kuwepo kwa mfumo wa haki ya madai ambao unazingatia haki kwa mujibu wa Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatoa msisitizo katika:-

I. Kutenda haki kwa wote bila ya kujali hali ya mtu kijamii au kiuchumi;
II. Kutocheleweshe haki bila sababu ya kimsingi;
III. Kutoa fidia ipasayo kwa watu wanaoathirika kutokana na makosa ya watu wengine na kwa mujibu wa sheria mahususi iliyotungwa na Bunge;
IV. Kukuza na kuendeleza usuluhushi baina ya wanaohusika katika migogoro.

Matatizo yaliyopo kwenye Mfumo wa Haki ya Madai Tanzania.

- Sheria zilizopo sasa zinazohusu mwenendo wa madai, kama vile, Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai ni ngumu kueleweka hasa kwa wale ambao hawajasoma fani ya sheria.
- Sheria zilizopo sasa zinazohusu mwenendo ya madai, hazielezi ni nini wadaawa wanatakiwa kufanya kabla ya mashauri kuanza kusikilizwa.
- Utaratibu wa kuongeza muda wa kupeleka utetezi haupo wazi na hivyo kusababisha kucheleweshwa kusikilizwa kwa mashauri.
- Hakuna kanuni za kisheria zinazoeleza uwezo wa Mahakama juu ya kuongeza muda wa kupeleka utetezi;
- Kiwango cha ucheleweshwaji wa kupeana nyaraka kupitia Mahakama ni tatizo ambalo husababisha msongamano wa mashauri ya madai Mahakamani.
- Uendeshaji wa mashauri ya madai ni wa gharama sana kwa Watanzania walio wengi hasa kutokana na kucheleweshwa kusikilizwa kwa mashauri hayo.
- Mfumo wa haki ya madai haueleweki na kwa kawaida ni vigumu kujua mashauri hayo yatagharimu kiasi gani cha fedha na ni kwa muda gani.
- Mara nyingi ni vigumu kwa wadaawa kuelewa mwenendo na taratibu za Mahakama. Mfumo uliopo ni wa upinzani sana na mara nyingi muda wa mashauri kuisha hutegemea wadaawa wenyewe.

Usuluhishi wa Migogoro kama Tatizo

- Usuluhishi wa migogoro haujawa na mafanikio kama ilivyotegemewa katika kuharakisha/kuchochea makubaliano katika kutatua migogoro pamoja na ukweli kwamba Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri

ya Muungano ya Tanzania inazitaka Mahakama kuhimiza na kusaidia njia za amani katika kutatua migogoro. Misingi ya usuluhishi imesimikwa kwenye vifungu vya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai vinavyohusiana na usuluhishi wa migogoro na pia kwenye vifungu vya Sheria ya Usuluhishi (Arbitration Act).

- Maafisa wachache wa Mahakama ndio wenye ujuzi wa usuluhishi wa migogoro.

- Mawakili wengi hawapendi usuluhishi wa migogoro kwa sababu ya kinachodaiwa kuwa njia hii ina malipo kidogo, hivyo, hawashiriki ipasavyo katika kuwahimiza wateja wao kushiriki katika usuluhishi wa migogoro yao.

- Usuluhishi pia umekuwa na matatizo kwa sababu wakati mwingine maafisa wa Mahakama wamekuwa wakitenda wajibu huo kwa kujiweka kwenye mamlaka kama Majaji na Mahakimu, kuliko nafasi ya wasuluhishi.

- Maafisa wa Mahakama wana mtazamo kuwa, usuluhishi wa migogoro ni mzigo mwingine ulioongezwa kwao pamoja na majukumu mengine waliyonayo.
- Ulazima wa usuluhishi umekuwa ukitajwa kuwa kitu kinachochangia katika ucheleweshaji wa kesi wakati wahusika katika kesi hizo wanapokuwa hawana moyo wa kufanya usuluhishi na hivyo huhudhuria usuluhishi kwa kuwa tu ni jambo la utaratibu wa Mahakama.

- Nafasi mbili ambazo Mahakama inazo; kama msuluhishi na mwamuzi hazijaeleweka vizuri kwa wahusika wa mashauri. Kwa hiyo, katika macho ya wenye kesi, wajibu wa Majaji na Mahakimu katika usuluhishi na katika kuendesha kesi haiwezi kutofautishwa kirahisi.

Jaji wa Mahakama ya Rufaa Mh. Kalegeya (wa kwanza kulia) na Wakili wa kujitegemea Felix Kibondya (wa kwanza kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja na mtaalam wakati wa kujadili waraka wa Majumuisho wa mradi wa mfumo wa madai.

- Wadaawa hupeleka mashauri yao Mahakamani kama hatua ya mwisho kwani katika hali ya kawaida, ni lazima wanakuwa wamejaribu kufanya usuluhishi na upatanishi na kushindikana kabla ya kwenda Mahakamani. Kwa hiyo, kwa wahusika wa kesi kuwa na utayari wa jitihada za kuwa na usuluhishi mwingine (sasa katika Mahakama) inachukuliwa kama ni kupoteza muda.

Sheria na Kanuni Zinazorekebishwa Chini ya Marekebisho ya Mfumo wa Madai.

Zifuatazo ni Sheria na Kanuni zinazorekebishwa chini ya mfumo huo:-

- Sheria ya Mahakimu [Sura ya 11 ya Marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ya Ukomo [Sura ya 10 ya Marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai [Sura ya 33 ya Marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ya Usuluhishi [Sura ya 15 ya marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ya Ushahidi Tanzania [Sura ya 6 ya marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Serikali [Sura ya 5 ya marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ya Mamlaka ya Rufaa [Sura ya 141 ya marekebisho ya mwaka 2002].
- Sheria ya Mabaraza ya Kata [Sura ya 7 ya marekebisho ya mwaka 2002].
- Kanuni za Mahakama ya Rufaa Tanzania; Tangazo la Serikali Na.102 la mwaka 1979.
- Kanuni za Mwenendo wa Mashauri ya Serikali (na taratibu); Tangazo la Serikali Na.376 la mwaka 1968.
- Kanuni mbalimbali zilizotungwa chini Sheria ya Usimamiaji Haki na Matumizi yake (Judicature and Application of Laws) [Sura ya 1 kama sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002] ambazo ni pamoja na:-

    - Kanuni za Muonekano wa Maafisa wa Serikali; Tangazo la Serikali Na.306 la mwaka 1964.

    - Kanuni za Likizo za Mahakama; Tangazo la Serikali Na. 307 la mwaka 1964.

    - Kanuni za Ada ya Mahakama; Tangazo la Serikali Na.308 la mwaka 1964.

    - Kanuni za Mwenendo wa Madai (kwa Rufaa za Mashauri yaliyoanzia Mahakama za Mwanzo); Tangazo la Serikali Na.312 la mwaka 1964.

    - Kanuni za Madalali wa Mahakama na Wahudumu (Uteuzi, Mishahara na Nidhamu); Tangazo la Serikali No. 315 la mwaka 1997.

- Kanuni za Masjala za Mahakama Kuu; Tangazo la Serikali Na. 164 la mwaka 1971.

- Kanuni za Lugha ya Mahakama; Tangazo la Serikali Na. 115 la mwaka 1981.

- Kanuni za Mahakama ya Biashara (ada); Tangazo la Serikali Na. 275 la mwaka 1999.

Hatua za Mapitio ya Mfumo wa Haki ya Madai
Mfumo wa Haki ya Madai unafanyiwa kazi kwa kufuata hatua zifuatazo:-

- Hatua ya kwanza; Maandalizi ya Waraka wa Majumuisho ya Awali (Position Paper); ambayo yalianza kwa kuandaa wazo kuu la hali halisi.
- Hatua ya pili; ilihusika na kufanya mikutano na wadau wakuu muhimu wenye kutoa maamuzi kwenye sekta ya sheria wakiwemo; Jaji Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Msajili wa Mahakama ya Rufaa, Wasajili wa Mahakama Kuu na Mtendaji Mkuu wa Kitengo cha Kanuni Bora (BRS) ambayo iliandaliwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania.
- Hatua ya Tatu; katika hatua hii wadau mbalimbali walishirikishwa katika kutoa maoni yao juu ya Waraka wa Majumuisho ya Awali (Position Paper). Mchakato huo ulifanyika kwa njia ya; warsha, semina pamoja na kukusanya hoja zilizokwishaandikwa na wadau kwenye eneo hili, wakiwemo Majaji, Mahakimu, Mawakili wa Serikali na Mawakili wa kujitengemea. Haya yalifanyika katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Mbeya.
- Hatua ya Nne; inahusika na kufanya mapitio ya sheria na kanuni zilizoorodheshwa hao juu, ikiwa ni pamoja na kutayarisha rasimu ya sheria na kanuni hizo na pia kuandaa Taarifa ya mwisho katika zoezi hili. Taarifa hiyo itawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali/Waziri wa Katiba na Sheria. Hatua hii inafanyiwa kazi na mtaalam aliyeajiriwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania.

MAENEO YA MKAZO WAKATI WA KUTAFUTA MAONI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliandaa warsha mbalimbali kwa ajili ya wadau tofauti ili kupata maoni juu ya mfumo ulipo wa haki ya madai. Wadau hao ni: - Majaji wa Mahakama ya Rufaa, Majaji wa Mahakama Kuu, Mahakimu, Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea ili kujadili maeneo mbalimbali yaliyotambuliwa Waraka wa Majumuisho ya Awali (Positon Paper) ambayo ni:-

- Makubaliano ya Awali (Pre-action Protocols).
- Usuluhishi wa Migogoro.
- Kufanya uendeshaji wa mashauri kuwa wa upinzani kidogo.
- Kurahisisha uendeshaji wa mashauri.
- Kanuni ya mwenendo na maadili ya mawakili.
- Kurekebisha utawala na muundo wa mfumo wa Mahakama.

Mh. Jaji Mkuu na baadhi ya majaji wa Mahakama ya Rufaa na mahakama Kuu wakijadili waraka wa majumuisho (Position Paper) wa mfumo wa madai Tanzania.

Makubaliano ya Awali (Pre-action Protocols)
Imependekezwa kuwa; hatua za lazima zichukuliwe kwa kushirikiana na wenye nia katika masuala ya biashara, wanataaluma, wadau pamoja na makundi mengine katika kuandaa makubaliano ya awali yanayofaa katika mazingira ya Tanzania, kwa nia ya kuweka viwango vya kawaida katika makubaliano ya awali yatakayofanyika kuhusiana na aina fulani za mashauri. Hivyo imependekezwa kwamba;

- Makubaliano ya awali yasishughulikiwe na Mahakama.
- Muda utakaokuwa umetumika katika makubaliano ya awali usihesabike wakati wa kuhesabu muda kwa mujibu wa Sheria ya Ukomo.
- Wadaawa wawe na haki ya kuwakilishwa na Mawakili au mtu mwingine yeyote.
- Sheria iwalazimishe wadaawa kusajili Mahakamani mikataba itokanayo na makubaliano ya awali, tayari kwa utekekelezaji sawa na ilivyo katika hukumu iliyoridhiwa na wadaawa.
- Mawakili wanaowapotosha wateja wao katika makubaliano ya awali wahukumiwe kulipa gharama katika shauri hilo.
- Makubaliano ya awali lazima yaendeshwe na wataalam katika eneo hilo/husika.
- Mamlaka ya kifedha ya Mahakama katika kusajili mikataba ya makubaliano ya awali lazima iwekwe wazi.

Usuluhishi wa Migogoro
Imependekezwa kwenye mapitio ya mfumo wa haki ya madai kuwa:-

- Mfumo wa usuluhishi wa migogoro usifanywe na Mahakama bali na wanataaluma binafsi wa eneo la usuluishi na upatanishi.
- Mahakama ziwajibishwe kisheria kutumia majaribio ya tathmini ya kesi zisizopingamana (test of neutral

case evaluation) ili kuweza kuamua kesi inayofaa kwa ajili ya mchakato wa usuluhishi. Hii itajumuisha kuwa na mawakili waandamizi wawili au zaidi watakaotoa maoni yako kwa maandishi juu ya majukumu katika kesi baada ya kuzipitia na kuzielewa hati za kesi husika pamoja na sheria zake.

- Mawakili wanaowakilisha wateja wao kwenye usuluhushi wanaweza kupata taarifa ambazo wadaawa wanaweza wasizionyeshe kwenye kesi ambayo inaendeshwa kwa njia ya kawaida mpaka mwisho mahakamani.
- Kesi ambazo hazikufanikiwa wakati wa makubaliano ya awali (pre-action-protocols) zitapangwa kwenye usuluhishi pale tu panapokuwepo mazingira maalum. Aidha, mkutano wa awali katika usuluhishi pamoja na usuluhishi wenyewe lazima vifanyike kwa pamoja ili kuokoa muda/kuepuka kupoteza muda.
- Kuna hitajio la kutunga/kutengeneza kanuni na sera za kusimamia na kulinda usuluhishi wa migogoro kwa ufanisi zaidi; hata hivyo, si lazima kanuni hizi zitungwe kwenye sheria tofauti.
- Kuanzishwe taasisi maalum ya kuendesha mafunzo ya usuluhishi wa migogoro kwa watumishi, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umma juu ya usuluhishi wa migogoro.

Kufanya Uendeshaji wa Mashauri kuwa wa Upinzani Kidogo

Imependekezwa kuwa;

- Mawazo ya usuluhishi wa migogoro ambayo yanatumika sasa kwenye Mahakama zetu yatumike katika uendeshaji wa mashauri.
- Majaji na Mahakimu lazima watumie ipasavyo mamlaka walizopewa na Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai pamoja na kusimamia mwenendo wa Mahakama.

Kufanya Mashauri kuwa Rahisi

Imependekezwa kuwa:-

- Mahakama izingatie daima Ibara ya 107(2)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inakataza umalizaji wa mashauri katika misingi ya taratibu za kiufundi (technicalities).
- Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sheria ya Ushahidi Tanzania na Sheria ya Mahakimu zitafsiriwe katika lugha ya Kishwahili.
- Majaji, Mahakimu na Mawakili wapunguze matumzi ya maneno ya kilatini kwenye Mahakama.

Kupunguza Muda wa Uendeshaji Mashauri

Imependekezwa kuwa:-

- Kanuni ya siku sitini (60) iwekwe kuwa ndicho kiwango cha juu kwa kuahirisha kesi.
- Wakili atakayeombwa kumsaidia wakili mwenzake katika kesi, lazima ajiandae kuendesha shauri husika.
- Muda maalumu wa kuwasilisha hati za mashauri pamoja na kumaliza mashauri lazima upunguzwe.
- Kuna umuhimu wa kuanzisha Mahakama maalum (specialized court) na pia zipatiwe wafanyakazi wenye uwezo kwenye eneo lake mfano: Mahakama za familia, ardhi, biashara n.k.
- Utendaji wa maafisa wa Mahakama lazima ufanyiwe tathmini pamoja na uwepo wa vipindi vya kuwapima ili kuboresha utendaji wao.
- Matumizi ya huduma za kieletroniki za kupeleka hati zinazohusiana na kesi kwa mdaawa zitumike ili zijumuishwe na huduma mbadala za kupeleka hati za mashauri.

Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Mhe. Jaji Prof. Ibrahim Juma (wanne kushoto)akiwa na wadau wa sekta ya sheria wakiongozwa na Jaji Mkuu (watano kushoto) baada ya mkutano wa kujadili Waraka wa Majumuisho wa Mfumo wa Madai.

Maboresho ya Utawala na Mfumo wa Mahakama

- Kuboresha Miundombinu ya Mahakama na ujira wa Majaji, Mawakili wa Serikali na watumishi wengine wa Mahakama ili kutimiza matarajio ya wadaawa.
- Kuwepo kwa kanuni za utendaji kazi kwa watumishi wa Mahakama, Madalali wa Mahakama na Washauri wa Mahakama. Washauri wa Mahakama wanatakiwa waapishwe kabla ya kupewa kazi (kuanza kazi)
- Mabaraza ya Kata yanatakiwa yahusishwe na mfumo wa Mahakama.
- Kuboresha masharti na mikataba ya kazi kwa Majaji, Mahakimu na makarani wa Mahakama ili kuwapa motisha na kuongeza ufanisi. Vilevile malipo (ujira) wanayopata watumishi wa Mahakama yanatakiwa yawiane na malipo (ujira) wanayopata watumishi wa Serikali na Bunge.
- Ili kuweza kulinda uhuru wa Mahakama, watumishi wa Serikali wakiwemo wakuu wa Mikoa hawatakiwi kuwemo kwenye Kamati za Nidhamu dhidi ya maafisa wa Mahakama.
- Huduma za Mahakimu Wakazi wenye mipaka ya nyongeza (Extended Jurisdiction) zitumike zaidi ili kupunguza msongamano wa kesi kwenye Mahakama Kuu na malipo yao yalingane na malipo ya Majaji wa Mahakama Kuu.
- Kumbukumbu za Mahakama zinatakiwa kutilia maanani maandishi ya wasioona. Juhudi pia zifanyike kuwajali watu wengine wenye mahitaji maalumu.

Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

- Jukumu la kuchapisha vitabu vya kumbukumbu za kesi lipewe taasisi inayojitegemea na siyo idara ya Mahakama.

Kuwepo kwa miundombinu muhimu ya teknolojia ya kuandikisha nyaraka za mashauri kwa njia ya kielekitroniki na mawasiliano ya elekitroniki kwa watumishi wa Mahakama (maafisa wa Mahakama)

MAPITIO YA KANUNI ZA MAHAKAMA YA RUFAA ZA 1979

Kanuni za Mahakama ya Rufaa ni miongoni mwa kanuni zilizopangwa kufanyiwa mapitio. Kanuni hizi ziliandaliwa mwaka 1979 wakati masjala ya Mahakama Kuu ikiwa moja, Majaji wachache na pia wadaawa walikuwa wachache. Kwa muda mrefu Majaji wamekuwa wakitoa maoni dhidi ya kanuni hizi kupitia maamuzi mbalimbali ya Mahakama. Upungufu na matatizo yaliyokuwepo kwenye kanuni hizo yalikuwa ya kidhihirishwa na Majaji katika maamuzi mbalimbali ya kesi.

Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania wakati akifungua mkutano wa Majaji wa mahakama ya Rufaa kujadili waraka wa Majumuisho wa Kanuni za Mahakama ya Rufaa za 1979. Aliyekaaa kulia ni Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na kushoto ni Dkt. Mapunda

Mchakato wa mapitio na kurekebishwa kwa Kanuni hizo yalianza mwaka 2009 ulianzishwa na mtaalam ambaye alipewa kazi ya kuandaa maelezo ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa za mwaka 1979 zilivyo pamoja na changamoto zake. Baada ya kuandaa maelezo hayo Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliandaa muhtasari wa majadiliano na kuwashirikisha wadau mbalimbali kujadili, kutoa maoni yao na mapendekezo juu ya Kanuni hizo. Wafuatao ni wadau walioshirikishwa kutoa maoni hayo:-

1. Majaji wa Mahakama ya Rufaa
2. Kamati maalum ya Majaji wa Mahakama ya Rufaa
3. Majaji wa Mahakama Kuu
4. Mawakili wa Kujitegemea na Mawakili wa Serikali Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.
5. Vitivo vya Sheria vya Vyuo Vikuu, Asasi zisizo za Serikali na zile zinazotoa msaada wa kisheria.

Baadhi ya Majaji wa Mahakama ya Rufaa Tanzania wakiwa katika picha ya pamoja na Wanasheria wakati wa mkutano wa kujadili majumuisho ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa za 1979.

Matatizo ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa za Mwaka 1979

Malalamiko makubwa yalihusu kucheleweshwa kwa kesi, gharama za kesi na ugumu katika kukata rufaa. Baadhi ya malalamiko hayo yamesababishwa na kanuni zenyewe, wakati malalamiko mengine yako nje ya mipaka ya Mahakama ya Rufaa ikiwemo upungufu wa Majaji wa Mahakama ya Rufaa, upungufu wa fedha za kuendeshea Mahakama hiyo, uchache wa wafanyakazi, miundombinu na misaada mingine ya kitaalamu, kwa mfano;-

- Muda wa siku kumi na nne (14) wa kuwasilisha taarifa ya nia ya kukata rufaa kwa Msajili wa Mahakama Kuu baada ya maamuzi ni mfupi sana, pamoja na muda wa siku saba (7) wa kuujulisha upande mwingine kuhusu kuwepo kwa taarifa ya nia ya kukata rufaa ni mfupi hasa kama muda huo utaingiliwa na siku za mapumziko.
- Maombi ya kusimamisha utekelezaji wa hukumu hayako wazi, haifahamiki kama kusitishwa ni moja kwa moja baada ya taarifa ya kukata rufaa au lazima kupeleka maombi ya kusimamisha.
- Muda wa kupokea pingamizi za awali ni mfupi.
- Vigezo vya kupinga maamuzi ya Jaji mmoja wa rufaa haviko wazi kwenye Kanuni husika hivyo, kuleta ugumu wa kutoa pingamizi au kuwepo kwa njia inayofanana inapotakiwa kufanya pingamizi.
- Kutokuwepo kwa usawa, kufanana na umakini kati ya Majaji wa Mahakama ya Rufaa katika kutumia Kanuni dhidi ya kusimamisha utekelezaji wa hukumu baada ya kuwepo kwa rufaa. Kiutendaji, kutoa taarifa ya kusudio la kukata rufaa siyo kinga ya kuzuia kutekeleza hukumu. Amri ya kukaza hukumu iko wazi kutekelezwa mpaka pale ambapo upande mmoja umeomba kusimamisha utekelezaji na ombi kukubalika.
- Kutokuwepo kwa umakini wa kushughulikia maombi ya muda wa nyongeza, Kanuni zinaelekeza upande unaotoa maombi uonyeshe ama utoe sababu za kina ambazo zitakubalika na Mahakama. Kanuni hazionyeshi wazi ni sababu gani za msingi katika

kuongeza muda.

- Hitaji lisilo la lazima la kujumuisha nakala ya amri katika kukaza hukumu au amri katika kumbukumbu za rufaa mbali na uwepo wa nakala ya hukumu ambayo ni chimbuko la amri ya kukaza kuhumu.
- Kutokuwepo na kanuni inayotoa haki ya kujibu hoja zilizojitokeza kutoka kwenye majibu ya kiapo.
- Hakuna kanuni inayoruhusu kuahirisha usikilizaji maombi wala inayotoa maelekezo nini kifanyike endapo Jaji wa Mahakama ya Rufaa atastaafu au kufariki.
- Kutokuwepo kwa kanuni inayoelekeza nini kifanyike iwapo mdaawa atafariki.

Marekebisho ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa za 2009

- Kanuni mpya zimeelekeza kuwepo kwa hoja za maandishi katika rufaa. Wahusika wanatakiwa waandae hoja za maandishi na kuzipeleka masjala ya Mahakama ya Rufaa ndani ya siku sitini (60) baada ya kuwasilisha rufaa mahakamani au taarifa ya maombi, kulingana na shauri lilivyo. Hoja za maandishi inabidi ziandaliwe kwa umakini kwani Mahakama ina mamlaka ya kukataa hoja za maandishi ambazo zinaonekana haziko wazi, hazina uhakika na ina mlolongo mrefu bila ya sababu. Upande mwingine inabidi upelekewe nakala ya hoja za maandishi ndani ya siku kumi na nne (14) tangu hoja zilipopokelewa masjala, naye anatakiwa aandae na kupeleka majibu ya hoja hizo masjala ya Mahakama ya Rufaa ndani ya siku thelathini (30) tangu alipozipokea toka kwa upande mwingine. Wakati wa kusikiliza maombi au rufaa, pande husika zitapewa nusu saa tu ya kutoa maelezo ya hoja kama Mahakama itaona kuna haja ya kuwataka wahusika wafanye hivyo.
- Kuwepo kwa hoja za maandishi, kutapunguza mahitaji ya kuwa na kanuni itakayoelekeza kuahirishwa kwa shauri.
- Kanuni mpya zimeongeza muda wa kutoa taarifa ya rufaa kutoka siku kumi na nne (14) hadi siku thelethini (30) kuanzia siku maamuzi yanayokatiwa rufaa yalipotolewa. Na muda wa kupeleka nakala kwa wahusika wa rufaa umeongezwa kutoka siku saba (7) na kuwa siku kumi na nne (14) tangu taarifa ya rufaa ilipopokelewa Mahakamani.
- Kwa sasa muda maalum umewekwa kwa wanaotaka kutoa pingamizi la awali wakati wa kusikiliza rufaa. Mhusika anatakiwa atoe taarifa ya kusudio la kutoa pingamizi siku tatu kabla ya kusikilizwa kwa shauri, akitoa sababu za pingamizi hilo. Nakala tano (5) za pingamizi lazima ziwasilishwe kwa Msajili wa Mahakama ya Rufaa pamoja na nakala za sheria na maamuzi yatakayotumika katika pingamizi lazima yambatishwe na taarifa ya pingamizi.
- Zimeongezwa fomu mpya za taarifa za rufaa ambazo zinatakiwa zijazwe na mkata rufaa ambaye yuko gerezani. Fomu B/1 na C/1 ambazo zinamtaka mkata rufaa kutaja tarehe ya hukumu na kutiwa hatiani, tarehe ya kuingia gerezani na tarehe ya kuitoa taarifa ya rufaa.
- Kuhusu taarifa za nyongeza za rufaa, mrufani au mrufaniwa anatakiwa apeleke masjala ya Mahakama ya Rufaa nakala nane (8) za taarifa hizo zikiambatana na nyaraka au sehemu ya nyaraka, ambazo kwa maoni ya mhusika, zinatakiwa kwa maamuzi ya rufaa.
- Nakala (8) za orodha ya kesi zilizoamuliwa au machapisho kuhusiana na suala husika ambayo mrufani au mrufaniwa ataitumia wakati wa kusikiliza rufaa zinatakiwa ziwasilishwe masjala ya Mahakama ya Rufaa, orodha hiyo ijumuishe ukurasa husika wa kitabu au makala au nakala ya kesi au kesi zikiwa na namba za kesi, majina ya kesi yakionyesha namba na mwaka kesi hiyo ilipoamuliwa. Kama ni nukuu kutoka kwenye vitabu, basi yaandikwe majina ya watunzi na matoleo ya vitabu. Orodha hii lazima ipelekwe kwa wahusika wengine katika rufaa.
- Mahakama ya Rufaa imepewa mamlaka ya kuongeza muda wa ukomo katika maombi bila ya kujali asili ya maombi hayo ama chanzo.

Baadhi ya Majaji wa Mahakama kuu ya Tanzania na ZNZ na Wanasheria wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa mkutano wa kujadili waraka wa Majumuisho ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa. Wa pili kushoto ni Mwenyekiti wa Tume ya kurekebishs Sheria Tanzania Mhe. Jaji Prof. Ibrahim Juma.

MAFANIKIO YA MAPITIO YA MFUMO WA HAKI ZA MADAI

Tangu mradi huu ulipoanza mwaka 2006, kumekuwa na mafanikio yafuatayo:-

- Kutengenezwa kwa Waraka wa Majumuisho ya Awali (Position Paper) ya mfumo wa Haki za Madai nchini Tanzania pamoja na mapendekezo kwa ajili ya maboresho.
- Mapitio ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa za 1979, mapitio ambayo yamewezesha kuwepo kwa marekebisho kwenye Kanuni za Mahakama ya Rufaa za mwaka 1979 na kuwepo kwa Kanuni mpya za Mahakama ya Rufaa za mwaka 2009.
- Kupatikana kwa mtaalam ambaye anayafanyia kazi maelezo ya hali halisi ya mfumo wa Haki za Madai na baadae kutoa Rasimu ya Taarifa ya marekebisho ya sheria na kanuni zinazohusika ili kurekebisha matatizo yaliyoonekana katika mfumo wa haki za madai.